

Maswali

1. Mbona Esau aliuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza?
2. Isaka alitaka Esau afanye nini?
3. Nani alisikia mazungumzo ya Isaka?
4. Rebeka alimuambia Yakobo afanye nini?
5. Rebeka alimuambia Yakobo afanye nini wakati akimuendea Isaka?
6. Yakobo alisema uongo upi wakati alimuendea Isaka.
7. Isaka alibariki nani?
8. Mbona Esau alimchukia Yakobo?

Majibu

1. Esau aliuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya njaa.
2. Isaka alitaka Esau alete nyama ya mwituni atengeneze kitoweo.
3. Rebeka alisikia mazungumzo ya Isaka.
4. Yakobo aliambiwa alete mbuzi wa kitoweo.
5. Rebeka aliambia Yakobo avae ngozi ya mbuzi na nguo ya Esau.
6. Uongo ulikuwa “Mimi ni Esau.”
7. Isaka alimbariki Yakobo.
8. Kwa maana Yakobo alimdanganya Isaka na akabarikiwa.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

9 Yakobo na Esau

Marejeo

Mwanzo 25: 29 – 34 + 27

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu na ahadi zake ni mambo ya muhimu maishani mwetu.



Maneno maalum

1. Wana mapacha + Esau + Yakobo
2. Baraka za Mungu + Pacha mdogo Yakobo
3. Kitoweo + Choka + Haki ya mzaliwa wa kwanza + Uza
4. Isaka mzee + Nyama ya mwitu + Esau anawinda + Mbuzi 2 + Unywele + Ngozi ya Mbuzi+ Uongo + Barikiwa.
5. Amesha kula + Bariki pia + Esau anamchukia

9.1 Isaka na Rebeka walipoona kwa miaka mingi, Rebeka akajaliwa kupata watoto mapacha. Majina yao waliitwa Esau na Yakobo. Hao pacha walipokua wakawa watu wa aina tofauti sana. Esau alikuwa mwekundu mwenye malaika (unywele). Akakua na kuwa mwindaji. Alipenda kazi ya kuwinda, kupanda na kukimbia. Alipenda kuishi vilimani na kwenye msitu. Alifurahia kufanya uchunguzi wakati akiwinda. Esau aliwapatia jamaa yake nyama iliyotokana na – swala, ngiri, ndege na samaki. Yakobo alipenda kukaa nyumbani. Alikuwa mkulima. Alichunga wanyama na mifugo ya baba yake. Labda alilima ardhi kwa ajili ya kupanda ngano ya shahiri. Isaka alimpenda Esau, aliyemletea mawindo manono – nyama ya paa. Rebeka alimpenda Yakobo.

9.2 Mungu alimpa Ibrahimu ahadi nyingi ya Baraka. Hizi Baraka ziliendelea kushuka na kukabidhiwa kila kizazi, kwa mwana aliyeteuliwa na Mungu. Mungu alimwambia Rebeka ya kwamba pacha mdogo atakuwa na haki ya mzaliwa wa kwanza na Baraka. Yakobo alikuwa mdogo.

9.3 Siku moja alitoka kuwinda akaja nyumbani. Hakula chakula kwa siku kadhaa, hivyo alikuwa na njaa sana. Yakobo alikuwa akipika chakula cha dengu naye Esau akamuomba chakula kidogo ale. Yakobo alitaka haki ya kuzaliwa. Esau alisikia harufu nzuri ya chakula kilipokuwa kikipikwa. Alijisikia njaa sana hata hakujali juu ya haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Alikubali ya kwamba atampa hiyo nafasi ya mzaliwa wa kwanza, kwa kubadilishana na chakula.

9.4 Miaka mingi baadaye Isaka akawa mzee, mgonjwa na macho mazito kuweza kuona. Isaka alimwita Esau, akamtaka aende kuinda na kuwinda na amtengenezee chakula, mlo wa nyama.

Pia alimwambia Esau kwamba atakaporudi, atampa Baraka ya Mungu.

Rebeka alikuwa nje ya hema la isaka. Akamsikia alichosema Isaka. Rebeka alitaka Yakobo awe na huo mbaraka, kama Mungu alivyoahidi lakini Yakobo wala Rebeka hawakusubiri Mungu afanye mambo kwa jinsi yake. Mara Rebeka alimuita Yakobo. Akamtuma akatwae wanambuzi wawili. Rebeka akaandaa nyama ya mbuzi, chakula kitamu. Kwa makini sana akashona mikononi mwa Yakobo, katika viganja na katika shingo, kumfanya awe kama Esau. Yakobo akavaa nguo za Esau. Akajifanya ndiye Esau.

Mungu alikwisha sema ya kwamba ni Yakobo atakayekuwa na huo mbaraka. Siku zote Mungu anatumza ahadi zake. Rebeka aliposikia Isaka akiahidi kumpa Esau mbaraka, alifadhaika akatumia Yakobo amhadai Isaka.

Yakobo alimpelekea baba yake Isaka kitoweo. “Wewe ni nani mwanangu?” Isaka akauliza “Mimi ni mwanao Esau mzaliwa wa kwanza.”

Yakobo alidanganya. “Kula kitoweo nilichokutengenezea, na unibariki.” Isaka alihisi ngozi ya mbuzi kwa mikono ya Yakobo na akanusia nguo zake, “Sauti ya Yakobo,” Isaka alisema “Lakini mikono ya Esau.”

Isaka alikula kitoweo na akambariki Yakobo kwa ajili ya ahadi alizokuwa ameahidi Ibrahimu.

9.5 Baada ya Yakobo kuondoka Esau, alirudi, akampa babake isaka kitoweo. Isaka akaogopa na akatetemeka. “Nimesha kula kitoweo zamani,” Isaka alisema “Na nikambariki nduguyo Yakobo.” Esau alilia kwa uchungu. “Yakobo alikudanganya,” “Nibariki hata mimi pia, Oh baba.”

Esau alikuwa ameua haki ya mzaliwa wa kwanza kwa Yakobo. Kwa hivyo Yakobo akabarikiwa kwa ahadi za Mungu kwa Ibrahimu. Esau alimchukia Yakobo kwa sababu ya hizo Baraka. Esau akasema atamuua Yakobo baada ya baba yao kufa.

